TARIME MCHANGANYIKO SECONDARY SCHOOL
P.o box 86 Tarime- Mara-Tanzania (EA) Tel:+2557 68 901 641/+2557 84 471 566
Email:professormwerafoundation@gmail.com Website:professormwerafoundation.ac.tz

**18/09/2023**

***Kumb. Na. PMF/TMSS/2023/189***

Mzazi/Mlezi wa________________________________________Kidato cha_______

S.L.P _______________________________________________

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA TARIME MCHANGANYIKO KWA KIDATO CHA I, II, III NA IV MWAKA 2024**

1. Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.
2. Napenda kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha ____mwaka 2024.
3. Shule itafunguliwa tarehe____________Tunampa hongera sana kwa kupata nafasi hii
4. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni siku ya ufunguzi kwa ajili ya usajili.

Mwanafunzi asipofika shuleni siku saba (7) baada ya shule kufunguliwa, nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine walioko katika orodha ya akiba (Reserve list), ikumbukwe pia kuwa Jumamosi na Jumapili hatupokei wanafunzi.

**1. Maelekezo mafupi kuhusu shule:**

- Shule hii iko katika mtaa wa Uwanja wa Ndege kata ya Turwa, umbali wa kilomita mbili (2) kupitia barabara ya Nyamwaga kutoka stendi kuu ya magari mjini Tarime. Usafiri wa bodaboda kutoka stendi kuu mjini ni shilingi elfu moja (1000/=).
- Hii ni shule ya binafsi inayowalea wanafunzi wake kwa misingi na maadili ya kidini bila kubagua Imani ya dini yoyote
- Shule hii ni ya mchanganyiko (wasichana na wavulana) ina kidato cha I – IV na ni ya bweni na kutwa.
- Mbali na masomo tisa ya msingi - **English, Kiswahili, Basic Mathematics, Civics, History, Geography, Biology, Chemistry na Physics**, masomo ya **Information and Computer Studies (ICS)** na **Literature in English yanafundishwa pia.**

## 2. ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE 2023

| | BWENI ( BOARDING) | | | | KUTWA (DAY SCHOLARS) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F1 | F2 | F3F3 | F4 | F F1 | F2 | F F3 | F4 |
| **ADA** | 1,600,000 | 1,500,000 | 1,500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 |
| **Umisseta** | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| **Ukarabati** | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| **Afya/Tiba** | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| **Mahafali** | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 50,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 50,000 |
| **Mitihani ya Taifa** | | 20,000 | | 50,000 | | 20,000 | | 50,000 |
| **Mock Mkoa** | | 20,000 | | 20,000 | | 20,000 | | 20,000 |
| **Mitihani ya Nje** | | 50,000 | | 50,000 | | 50,000 | | 50,000 |
| **JUMLA** | **1,730,000** | **1,720,000** | **1,630,000** | **1,780,000** | **1,080,000** | **1,170,000** | **1,080,000** | **1,230,000** |

## 3. AWAMU ZA ULIPAJI ADA

Ada yote ya mwaka na michango italipwa kwa awamu nne kama ilvyoainishwa katika jedwali hapa chini

| | **BWENI ( BOARDING)** | | | | **KUTWA (DAY)** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **F1** | **F2** | **F3** | **F4** | **F1** | **F2** | **F3** | **F4** |
| **AWAMU YA KWANZA** *¼ Ada + Michango yote; ilipwe kabla au ifikapo* **tarehe 9/1/2023** | **530,000** | **595,000** | **505,000** | **655,000** | **330,000** | **420,000** | **330,000** | **480,000** |
| **AWAMU YA PILI** *¼ Ada ya 2; ilipwe kabla ya* **tarehe 10/4/2023** | **400,000** | **375,000** | **375,000** | **375,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** |
| **AWAMU YA TATU** *¼ Ada ya 3; ilipwe kabla ya* **tarehe 10/7/2023** | **400,000** | **375,000** | **375,000** | **375,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** |
| **AWAMU YA NNE ¼ Ada ya AWAMU YA 4** *¼ ya mwisho ya Ada; ilipwe kabla ya* **tarehe 15/9/2023** | **400,000** | **375,000** | **375,000** | **375,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** | **250,000** |
| **JUMLA** | **1,730,000** | **1,720,000** | **1,630,000** | **1,780,000** | **1,080,000** | **1,170,000** | **1,080,000** | **1,230,000** |

**ANGALIZO:**

1. Ulipaji wa ada na michango mingine utafanyika kwa awamu **NNE TU**.
2. Ikitokea mwanafunzi hajakamilisha ada kwa kufuata utaratibu, uongozi wa shule utamsimamisha masomo na kumrudisha nyumbani wakati wowote baada ya kutoa taarifa kwa mzazi/ mlezi.
3. Zingatia kuepusha usumbufu kwa mtoto.
4. Ada na michango mingine yote ilipwe katika **BENKI YA NMB. (Tawi lolote Tanzania) Jina la Akaunti: Tarime Mchanganyiko Secondary School. Akaunti Namba: 30410024119.** ***(Pesa taslim hazipokelewi shuleni)***

**4. MAHITAJI YA LAZIMA.**

**Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:-**

- Faili mbili (spring file) za kutunzia kumbukumbu zake
- Aje na picha nne (4) za passport
- Cheti cha kuzaliwa
- Awe na namba yake aliyofanyia mtihani wa kuhitimu elimu ya shule ya msingi
- Kitambulisho cha shule (***utalipia kitambulisho Tsh 5000/=shuleni)***
- Jembe jipya na mpini, fyekeo na ndoo (yenye ujazo wa lita 10 au 20)
- Mfagio wa ndani wenye mpini (soft broom) na wa nje wenye mpini (Chelewa)
- Bofa moja (Mathematical set)
- Bible (Revised Standard Version)
- Oxford Students Dictionary
- Counter book 12 Quire 2
- Madaftari mengine madogo 12 ya kufanyia mazoezi (Msomi)
- Sahani, bakuli, kijiko na kikombe kwa ajili ya chakula (kwa wote wa bweni na kutwa)
- Raba nyeupe zenye kamba kwa ajili ya michezo (Physical Education)
- Shati 2 nyeupe/Blauzi (Tomato) zenye mikono mifupi
- T –shirt yenye nembo ya shule (***utaipata shuleni kwa kulipia Tsh. 15,000/=)***
- Soksi nyeupe ndefu pea 2 kwa wasichana na kijivu kwa wavulana
- Begi la kubebea madaftari
- Rimu mbili kwa mwaka (Rimu moja kila muhula)

***4. Wanafunzi wa bweni waje na vifaa vifuatavyo:-***

- Godoro la 6' x 2 ½ (jipya kuepuka uambukizaji wa kunguni)
- Wenye tatizo la kukojoa kitandani washonee godoro lao plastki zisizopitisha mkojo
- Beseni la kuogea
- Shuka 2 – wavulana rangi ya bluu na wasichana rangi ya pink
- Mto (pillow) isiyofumwa na isiyokuwa na maua
- Taulo na ndala, ndala zisiwe yeboyebo au tairi
- Sanduku la bati imara la kuhifadhia vitu vyake lenye kufuli (lisiwe la mbao)
- Tochi.
- Blanket moja
- Neti ya mbu (Round net- blue au nyeupe)
- Galoni ya ujazo wa lita 3 au 5 kwa ajili ya maji ya kunywa
- Kiwi na brashi
- Sabuni za kuogea na za kufulia za kutosha
- Toilet paper za kutosha
- Mswaki na dawa ya meno
- Mafuta ya kujipaka (si vipodozi)
- Pesa za matumizi (Pocket money)
- Taulo za kike (Pads kwa wasichana)
- Kanga au Kitenge kwa wasichana
- Chupi za kutosha
- Iwapo vesti /blezia ni muhimu, vesti ziwe nyeupe na blezia ziwe nyeupe au nyeusi.

**SARE ZA SHULE KWA WAVULANA NA WASICHANA WA BWENI (BOARDING)**

***NB: Mahitaji yote yaliyo kwenye jedwali hapa chini yanapatikana shuleni***

| **Mahitaji (Wasichana)** | **Gharama** | **Mahitaji (Wavulana)** | **Gharama** |
|---|---|---|---|
| T-shirt Nyekundu | **5,000/=** | T- shirt Nyekundu | **5,000/=** |
| Sweta ya Blue | **15,000/=** | Sweta ya Blue | **15,000/=** |
| T-shirt ya Blue | **15,000/=** | T- shirt ya Blue | **15,000/=** |
| Shamba Dress | **20,000/=** | Shamba Shirt | **15,000/=** |
| Sketi Nyeusi | **22,000/=** | Suruali ya nyeusi | **22,000/=** |
| Sketi ya darasani (Jani la mgomba) | **22,000/=** | Suruali ya darasani ( Jani la mgomba) | **22,000/=** |
| Sketi (Penseli blue) | **22,000/=** | Suruali (Penseli blue) | **22,000/=** |
| Tracksuit | **25.000/=** | Tracksuit | **25,000/=** |
| **JUMLA** | **146,000/=** | **JUMLA** | **141,000/=** |

**SARE ZA SHULE KWA WAVULANA NA WASICHANA KUTWA (DAY)**

***NB: Mahitaji yote yaliyo kwenye jedwali hapa chini yanapatikana shuleni***

| **Mahitaji (Wasichana)** | **Gharama** | **Mahitaji (Wavulana)** | **Gharama** |
|---|---|---|---|
| Sweta | 15,000/= | Sweta | 15,000/= |
| T- shirt ya Blue | 15,000/= | T-shirt ya blue | 15,000/= |
| Sketi ya darasani | 22,000/= | Suruali ya darasani | 22,000/= |
| Tracksuit | 25,000/= | Tracksuit | 25,000/= |
| Sketi Penseli blue | 22,000/= | Suruali ya blue | 22,000/= |
| **JUMLA** | **99,000/=** | **JUMLA** | **99,000/=** |

**NB: Mavazi yaliyotajwa hapo juu ndiyo mwanafunzi ataruhusiwa kuwa nayo shuleni. Hatuhitaji nguo za ziada.**

***NB**** *Usafiri wa basi la shule upo kwa wanafunzi wa kutwa watakaouhitaji. Gharama yake kwa mwaka ni Tsh. 200,000/= Njia itakayotumika ni barabara kuu - Mogabiri, Tarime mjini, Magena hadi Mika.*

Pamoja na barua hii umeambatanishiwa:-

i) Sheria na kanuni za shule utakazofuata wakati wote uwapo shuleni
ii) Fomu ya kupima afya yako inayopaswa kujazwa kikamilifu na daktari anayetambulika kisheria kisha uje nayo siku ya kuandikishwa/kuripoti
iii) Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi/ Fomu ya mkataba wa kujiunga na Shule ya sekondari ya Tarime Mchanganyiko

Kumbuka kuja na barua hii ya wito wa kujiunga na shule wakati wa kuandikishwa /kuripoti'

***NB: Usajili utakuwa unaanza saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:00 jioni. Pesa zote za karo zilipwe benki. Hatupokei pesa taslimu shuleni. Pesa za mahitaji yako binafsi tu ndizo utakazokabidhi kwa msajili (makamu mkuu wa shule) kwa ajili ya kupewa mahitaji hayo yanayopatikana shuleni kwa mujibu wa barua hii.***

***"ELIMU BORA KWA MAISHA BORA YA BAADAYE"***

***KARIBUNI SHULE YA SEKONDARI TARIME MCHANGANYIKO***

**MWITA SAMSON MARWA**

**MKUU WA SHULE.**

**0629-396 450 / 0676-682451 (whatsapp)**

SCHOOL PRINCIPAL
05 OCT 2023
P.O. Box 86, TARIME
TARIME MCHANGANYIKO SEC. SCHOOL

*Kiambatanisho Na. 1*

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria za Shule ya Sekondari ya Tarime Mchanganyiko ni mwongozo na taratibu za namna ya kuishi kwa jamii iliyopo shuleni ili kufanikisha maendeleo ya shule ya Sekondari ya Tarime Mchanganyiko. Maendeleo ya shule hii yanategemea sana jinsi kila mmoja wa wanafunzi anavyozingatia sheria hizi.

- Sheria za Shule ya Sekondari ya Tarime Mchanganyiko ni kama ifuatavyo:

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama wazazi na walezi wake.
2. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuwaamkia walimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita au anapoingia darasani/katika mazingira ya shule.
3. Matusi na lugha chafu ni dalili ya kukosa heshima hivyo ni marufuku.
4. Mwanafunzi anatakiwa kutumia lugha ya kiingereza wakati wote awapo shuleni. Iwe darasani, bwenini, kwenye michezo na popote atakapokuwa katika maeneo ya shule.
5. Kila mwanafunzi sharti aoneshe mfano mzuri kwa watu wote. Yabidi awe mwenye adabu na mtii mbele ya walimu, watu wenye madaraka kama viranja wa shule, watumishi wasio walimu na watu wengine.
6. Kila mwanafunzi yabidi kuonesha bidii katika mafunzo ( masomo na kazi za uzalishaji mali au kazi zingine atakazohitajika kuzifanya). Uvivu hauna nafasi katika shule hii.
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa au kuchelewa.
8. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi kamwe hapa shuleni.
9. Wanafunzi wote sharti wavae sare ya shule wakati wote wa masomo. Wawapo shuleni au wawapo nje ya shule kwa ruhusa maalumu.
10. Kiburi, majibu ya jeuri, na matumizi ya lugha mbaya hairuhusiwi.
11. Kutii wito wa kengele kwa haraka inapogongwa. Hii ni muhimu kwa usalama wa shule na kufuata ratiba iliyopangwa. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kwenda mstalini akiwa anatembea.
12. Shule inatambua na kuheshimu uhuru wa kuabudu kwa kila mwanafunzi sambamba na sikukuu za kidini na kitaifa. Isipokuwa kama kutakuwa na shughuli za dharura, wanafunzi wote watashiriki bila kujali imani zao.

- Viongozi wa dini/ madhehebu wanaruhusiwa kuleta ibada shuleni lakini wanafunzi hawataruhusiwa kwenda kusali nje ya shule isipokuwa panapokuwa na sababu maalumu.

13. Kila mwanafunzi anatakiwa kujipenda yeye mwenyewe, awapende wenzake kama ndugu zake wa shuleni, awapende walimu kama wazazi wake, aipende shule kama nyumbani kwao, aipende na kujivunia nchi yake ya Tanzania na awe tayari kulinda mali za shule.
14. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujihusisha na mambo yafuatayo, vinginevyo atafukuzwa shule maramoja hata kama kosa ni la kwanza:

(a) Kutokuzingatia masomo, kufanya mitihani.
(b) Wizi
(c) Uasherati na ushoga
(d) Ubakaji
(e) Ulevi na matumizi yadawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, sigara .na vilevi vingine vya aina hiyo.
(a) Kupigana kupiga.
(b) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(c) Kudharau bendera ya Taifa.
(d) Kuolewa au kuwekwa kimada.
(e) Kubeba mimba.
(f) Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu au shule.
(f) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(g) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.
(h) Kutoroka shule/ kuwa nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu kutoka kwa mkuu au makamu mkuu wa shule, utalipia faini ya shilingi laki moja (100,000/=)

15. Ni lazima kuwahi darasani na kukaa kimya wakati wote.
16. Simu kwa ajili ya mawasiliano ya mwanafunzi kwa mzazi wake zipigwe katika ofisi ya mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule au mwalimu wa nidhamu pekee na sio vinginevyo.
17. Siku ya kutembelea wanafunzi (visiting Day) ni jumapili ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Shule haitaruhusu wageni kutembelea wanafunzi siku tofauti na iliyotajwa hapo juu labda kwa sababu maalumu.
18. Ni marufuku kuandika kwenye mbao za shule, madawati, kuta, sakafu n.k.

19. Matangazo yote ya wanafunzi sharti yahakikiwe kwa mwalimu mhusika kabla ya kubandikwa kwenye mbao za matangazo (notice board).

20. Ni marufuku kutembea au kukutwa karibu na sehemu zifuatazo:

(a) Sehemu zinazouza pombe(vilabu au baa)

(b) Majumba yote ya starehe.

(c) Nyumba za kulala wageni(Guest House)

(d) Makazi / mahali wanapoishi watumishi wa shule (walimu na watumishi wasio walimu).

21. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa nguo zinazobana na kuonesha maumbile yake ya ndani.

22. Ni marufuku mwanafunzi kunyoa kipara au minyoo mingine ya kihuni mfano kiduku pindi awapo shuleni au wakati wa likizo.

23. Ni marufuku kuvaa hereni au kuweka Curl kwenye nywele, kuvaa kanga, vitenge, kandambili na mavazi mengine ya aina hiyo.

24. Ni marufuku mwanafunzi kufuga nywele ndefu.

25. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Chakula chote kiliwe katika sehemu maalumu iliyowekwa kwa ajili hiyo.

26. Chakula kwa ajili ya wanafunzi kinapatikana shuleni. Hivyo hairuhusiwi kwa mwanafunzi au mzazi au mgeni yeyote kuja na chakula au vinywaji vya aina yoyote shuleni bila idhini / kibali maalumu.

27. Hairuhusiwi mwanafunzi kwenda jikoni wakati wa saa za masomo pasipo kibali maalumu.

28. Saa ya kulala kila mwanafunzi akae kimya na kulala. Baada ya kengele ya mwisho, pasiwepo na maongezi tena au kuzungukazunguka.

**USHAURI WA ZIADA:**

(a) Umekuja shuleni kwa lengo moja tu, kusoma.

(b) Ukizingatia na kufuata sheria za shule, utaishi vizuri na walimu wako watapata muda mwingi na hamu ya kukusaidia.

(c) Epuka vikundi vyenye nia mbaya ambavyo vinasababisha ushindwe kufikia malengo yako ya kitaaluma.

(d) Usifuate mkumbo ili usije kujuta baadaye.

(e) Kumbuka: Elimu yako itasaidia ukombozi wako binafsi, familia yako na taifa kwa ujumla. Hivyo tumia muda wako mwingi kujisomea kuliko kufanya vitendo visivyo na tija.

**TANIBIHI:** Uongozi wa shule unayo mamlaka ya kubadili kwa kuongeza au kuondoa baadhi ya sheria hizi ili ziendane na matakwa/ mahitaji ya wakati husika. Pia sheria zitakazotangazwa kwa mdomo zitakuwa na uzito sawa na zilizoandikwa.

*Kiambatanisho Na. 2*

# TARIME MCHANGANYIKO SECONDARY SCHOOL
## MEDICAL EXAMINATION FORM

**REQUEST FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

**TO BE COMPLETED BY A PHYSICIAN**

Ms_________________________________Age______________sex_________

I. Please examine the above as to his/her physical mental fitness for the pursuit of Secondary Education. This examination should include the following:-

A. Eye ________________________________________________

B. Hearing _____________________________________________

C. Limbs ______________________________________________

D. Speech _____________________________________________

E. Epilepsy_____________________________________________

II. A) Blood count ___________________________________________

B) Stool Examination______________________________________

C) Urine Analysis________________________________________

D) Syphilis and other V.D.R.L________________________________

E) T.B Test_____________________________________________

F) Pregnancy Test_______________________________________

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defectives or impairments, infections, chronic or incurable diseases e.t.c

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

_________

I certify that the above person is fit/is not fit to pursue secondary education as stated above

Signature ______________________________________

Designation _____________________________________

Station__________________________________________

Date __________________________Official Stamp

*Kiambatanisho Na. 3*

## MAKUBALIANO KATI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI NA UONGOZI WA SHULE:

### TAMKO LA MZAZI/MLEZI:

Mimi ______________________________________________ ambaye ni mzazi/mlezi wa ______________________________(mwanafunzi mtarajiwa) wa sanduku la barua (posta) ________________simu namba___________________ninayeishi ______ kitongoji cha __________________nimesoma sheria na maelekezo mengine ya shule yaliyo kwenye fomu hii na kwamba.

Nimekubaliana na maagizo na sheria hizo ili ziwe dira ya maisha ya mwanangu hapo shuleni pamoja na zile ambazo bodi ya shule, wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi itaona ni vema ziwe sehemu ya sheria za shule ya sekondari ya Tarime Mchanganyiko/. Aidha, nitahakikisha kuwa mwanangu anamaliza elimu ya sekondari na nitawajibika kwa kumlipia ada na michango mbalimbali ya shule pamoja na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

____________________ ________________________

Sahihi ya mazazi/mlezi Tarehe

### TAMKO LA MWANAFUNZI:

Mimi ____________________________________ ninakubaliana/ sikubaliani na sheria za shule ambazo zimeambatanishwa na barua yangu ya maagizo ya kujiunga na shule ya wasichana Tarime sekondari. Nimezisoma sheria hizo na kuzielewa bila shinikizo lolote lile kwa hiyo basi, mimi kwa hiari yangu mwenyewe nimeziafiki/ siziafiki na nitakuwa mtii/ siomtii wa sheria hizo pamoja na zingine ambazo bodi ya shule na wizara ya elimu na mafunzo zinafaa kuwa sheria za shule ya sekondari ya Tarime Mchanganyiko.

____________________ ______________________

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

**Je, ukipata matatizo ya dharura uongozi wa shule umuarifu nani?**

**______________________Uhusiano wako na yeye ____________________________________**



SCHOOL PRINCIPAL
05 OCT 2023
P.O. Box 86, TARIME
TARIME MCHANGANYIKO SEC. SCHOOL